# CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM)

## TAWI LA CHINA

Simu: +8613356857656
Barua Pepe: ccmchina001@gmail.com
China

Ofisi ya Katibu wa Tawi
Shangdong, Qingdao.

**RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TAWI KWA MWAKA 2024/2025**

**UTANGULIZI**

**Ndugu wana CCM na wanachama wa Tawi la CCM China,**

**Kidumu Chama Cha Mapinduzi.**

Awali ya yote napenda kumshukuru mwenyezimungu kwa neema ya afya na uzima, wale wagonjwa mola awape uponyaji wa haraka. Nitoe pia pole kwa watanzania wote pamoja na familia kwa kupatwa na msiba wa mwanafunzi mwenzetu Grace Mihuba aliefariki dunia kwa maradhi. Mungu ailaze pema roho ya marehemu Grace, ampe amani ya milele na mwanga wa milele amwangazie. Sisi wote ni wa Mwenyezimungu, na kwake ndio marejeo yetu.

Pili nitoe pole kwa ndugu jamaa na marafiki wote waliopoteza wapendwa wao kwa yaliyotokea Tanzania siku ya uchaguzi mkuu Oktoba 29, 2025. Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema.

Tatu nimshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kutafuta ufumbuzi wa swala hili ikiwemo kuundwa kwa tume ya uchunguzi, kutoa msamaha kwa wale waliokamatwa kwa kufata mkumbo, kuanzisha mchakato wa katiba mpya ndani ya siku 100 za kwanza tangu aingie madarakani, pamoja na kuanzisha wizara mpya ya vijana itakayoshughulikia na kutatua changamoto za vijana kwa ukaribu zaidi kuliko awali. Hii yote inaonyesha utayari na dhamira ya serikali kushughulikia yale yote yanayolalamikiwa na makundi mbalimbali nchini ikiwemo kundi la vijana.

Ndugu wana CCM Wenzangu na wanachama wa Tawi la CCM China.

Leo ninayo furaha kusimama mbele yenu kwenye mkutano mkuu wa tawi letu na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa shughuli za tawi kwa mwaka 2024/2025. Tumeshatimiza mwaka mmoja toka tuchaguliwe kama viongozi wa Tawi. Uongozi wetu uliingia madarakani Tarehe 31.11.2024 na kuanza majukumu yake rasmi. Katika utekeleaji wa majukumu ya kila siku ya tawi Uongozi uliunda kamati zitakazosimamia utekelezaji wa majukumu

mbalimbali pia kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu hayo. Kamati zilizoundwa zilipata baraka ya vikao vyote vya tawi na zilifanya kazi chiniya Halmashauri Kuu ya Tawi.Kamati hizo ni Kamati ya Elimu na Mafunzo; Kamati ya TEHAMA; na Kamati ya Uchumi na Fedha. Kila Kamati ilisimamiwa na mwenyekiti na Katibu wa Kamati husika.

Ndani ya muda tuliokaa madarakani ni mengi yamefanyika yanayoweza leo kuongelewa kama sehemu ya mafanikio au sehemu ya changamoto kwenye uongozi wetu.

**MAFANIKIO**

1. **KUSIMAMIA KATIBA**

   Tumejitahidi kwa kiasi kikubwa kusimamia katiba ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na miongozo mingine katika kuendesha shughuli za Tawi na Mashina yake. Mchakato mzima wa uchaguzi wa uongozi mpya unaofata baada yetu umefata taratibu za kichama na vikao vyote halali vya kimaamuzi. Huu ni utamaduni ambao tungependa kuuona unaendelezwa na uongozi ujao. Misingi ya chama ipo kwenye kufata kanuni, sheria na taratibu kwani wahenga wanasema 'Penye Sheria na Taratibu zitumike kwanza hizo ndipo busara ifate'.

2. **UHAMASISHAJI**
   Tawi limefanikiwa kutoa hamasa, kuelimisha wanachama juu ya ilani, na kusaidia kuwanadi wagombea wa Chama Cha Mapinduzi walioteuliwa kugombea nafasi mbali mbali kwenye uchaguzi uliopita wa Oktoba 29 kwa kuandaa Mabango au Posters za mara kwa mara zenye jumbe mbali mbali ikiwepo 'bango la salamu za mwenyekiti' ambalo lilikua linatoka kila jumatatu ya kila wiki, Bango la 'Ada ya Vyama Hunena, CCM NI KITENDO' lililokua linaelezea mambo yaliyofanywa na serikali ya awamu ya sita kwenye nyanja mbalimbali za maendeleo na bango la kuielezea ilani lililotoa elimu na uelewa wa wanachama juu ya ilani ya uchaguzi ya chama cha mapinduzi ya mwaka 2025 pamoja na mafanikio ya ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020.

3. **KUTOA KIPAUMBELE KWENYE MATUMIZI YA TEHAMA KWENYE SHUGHULI ZA TAWI**
   Kutoa kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA kwenye shughuli za Tawi. Kwa mwaka 2025, matumizi ya TEHAMA yalipewa kipaumbele kikubwa kwenye kuongoza shughuli zetu, kupashana habari, na kulitangaza Tawi letu nje ya mipaka ya China. Aidha, shughuli zote za Tawi na Mashina yake ziliripotiwa kwa usahihi na kwa wakati kwenye tovuti ya tawi, kurasa za kijamii ikiwemo facebook, Instagram, X, Tiktok, pamoja na magroup ya Tawi ya wechart na WhatsApp. Hii imesiadia katika kuwafikia wanachama wetu kwa urahisi na kunadi shughuli za Tawi na mashina yake kwa wakati. Aidha, tumefanikiwa kuanzisha Kamati mahusisi ya TEHAMA iliyosimamia kwa ukaribu shughuli hizi, hii ni pamoja na kuanzisha kurasa mpya ikiwemo ukurasa wa tiktok, whatsApp channel, na ukurasa wa X (Zamani Twitter).

4. **KUKAMILIKA KWA JARIDA LA TAWI**

Kukamilika kwa Jarida la Tawi. Jarida la Tawi ni wazo lililokuwepo kwenye vipindi viwili vilivyopita na kulirithi wazo hili kwenye uongozi huu unaomaliza muda wake. Kuundwa kwa kamati ya jarida kulipelekea kufanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa na kujitoa kwa wanakamati hadi kufanikiwa kukamilisha mchakato wa jarida letu ambalo wiki iliyopita tulilizindua kwa lugha ya kiswahili na leo tunazindua la lugha ya kingereza. Tunawaomba wanachama wote kulisoma na kulisambaza sehemu tofauti na kwa hadhira tofauti ili liwafikie watu wengi zaidi na shughuli za Tawi letu ziweze kufika mbali. Kukamilika kwa toleo la kwanza la jarida hili kunatoa nafasi ya kuanza kwa maandalizi ya toleo la pili hivyo viongozi wapya waone kwa namna gani watalianzisha wazo la toleo la pili hata kama halitakamilika kwenye uongozi wao ila muhimu ni kua na wazo kama sisi tulivyofanyia kazi kwenye wazo tulilolikuta.

5. **UIMARISHAJI WA KANZIDATA YA WANACHAMA**
Kwenye kipindi cha uongozi wetu, tumesimamia kuimarisha kanzi data ya Tawi kupitia mashina na kusajili wanachama kidigitali. Zaidi ya wanachama 200 wamesajiliwa kidigitali na kupatiwa namba za kielekroniki. Baadhi ya wanachama hao kadi zao za kielektroniki zimeshatoka na mawasiliano yanafanyika na CCM makao makuu kuona namna ya kuzifikisha kadi hizo kwenye tawi letu. Kufanikiwa kuboresha kanzi data kumesaidia kujua idadi ya wanachama hai kwenye kila shina na hivyo kurahisisha utambuzi wao na kurahisisha zoezi la uchaguzi wakati wa uchaguzi mkuu wa viongozi wa Tawi.

6. **KUUNDWA KWA KAMATI MUHIMU**
Kuundwa kwa mara ya kwanza toka historia ya Tawi kuanza kwa kamati muhimu za kimaamuzi kwenye ngazi ya Tawi ambazo ni **kamati ya usalama na maadili** pamoja na **kamati ya siasa ya tawi**. Kamati hizi zimezingatia katiba na miongozo mingine na zimekua msaada mkubwa kwenye uendeshaji wa shughuli za tawi.

7. **KUENDELEZA MADARASA YA ITIKADI NA UONGOZI**
Kuendeleza madarasa ya itikadi na uongozi. Tawi limefanikiwa kuratibu madarsa ya itikadi na uongozi kwa wanachama wake ikitumia uzoefu wa ndani na ikitumia wakufunzi kutoa nje ya tawi. Madarsa haya yamekua ni msaada kwa wanachama wapya kuijua, kuielewa na kuifanyia kazi itikadi sahihi ya Chama Cha Mapinduzi.

8. **ULIPAJI WA ADA**
Kupitia ushirikiano na mashina, uongozi umeendelea kuhamasisha wanachama kulipia ada za uanachama na kuchangia kwenye matukio ya muhimu ya kichama kwa ajili ya kukisapoti chama kuendesha shughuli zake. Hii ni kutokana na kutambua kua uhai wa chama ni wanachama na uhai wa wanachama ni kulipia ada za uanachama na kujitoa kwao kwenye shughuli za kichama.

9. **MUENDELEZO WA MAHUSIANO**
Tawi limeendelea kuimarisha uhusiano na wanachama na viongozi alumni walioongoza katika nafasi mbalimbali ndani ya tawi na ndani ya mashina kupitia vikao na walezi wa tawi na kupitia kurasa zetu za mitandao ya kijamii hasa kipindi cha uchaguzi mkuu ambapo Tawi la CCM China lilitoa idadi kubwa ya watia nia kwenye nafasi mbali mbali za uongozi kuliko tawi lingine lolote ya diaspora duniani, na baada ya vikao halali vya chama kufanyika Tawi limepata idadi kubwa ya wagombea wa kuchaguliwa majimboni pamoja na viti maalum hivyo kuendelea kulifanya Tawi letu kua tawi imara, lenye kuaminika

na linaloendelea kutoa viongozi makini na wenye weledi kuongoza katika ngazi mbalimbali ndani ya chama na serikali.

**10. UWAZI NA UWAJIBIKAJI**

Tawi limeandaa taarifa ya wazi ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/2025 kama taarifa inayojitegemea itakayoambatanishwa pamoja na taarifa hii ya utekelezaji. Hii ni hatua muhimu ya kuimarisha uwajibikaji wa rasilimali za chama na utawala bora.

**11. UHUISHAJI WA MASHINA**

Tawi limefanikiwa kuongeza idadi ya mashina na kufufua baadhi ya mashina yaliyolala kwa muda mrefu. Hii imepeleka kuongezeka kwa idadi ya mashina yaliyo hai kutoka mashina 14 kipindi tunapokea uongozi hadi mashina 17. Idadi kamili ya mashina haya inapatikana ukurasa wa 17 na 18 wa jarida la tawi kwa lugha ya kiswahili na ukurasa wa 16 na 17 kwa jarida la kingereza. Mashina haya ni pamoja na shina la Yunnan, Jinzhou, Chongqing, Jiangxi

**12. MIRADI**

Kupitia kamati ya mipango, uchumi na fedha tumefanikiwa kubuni, kutengeneza na kuuza T-shirts za chama kwa wanachama wetu. Huu ni mradi unaohitaji uungwaji mkono wa viongozi na wanachama kwani ukitekelezwa kwa ufanisi utakua ni moja ya njia ya kupata mapato yatakayosaidia kutekeleza shughuli za chama kwani Tawi na mashina yake hayana fungu la uendeshaji wa shughuli zake bali itategemea miradi iliyopo au kugharimia gharama za uendeshaji wa shughuli hizo kutoa vyanzo binafsi vya viongozi.

**13. KURATIBU MAPOKEZI YA KATIBU WA (NEC) SUKI**

Tawi kwa ushirtikiano na viongozi wa Shina la Beijing limefanikiwa kuratibu mapokezi ya Mjumbe wa Kamati Kuu (MCC) na Katibu wa (NEC), Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI) Ndugu Rabia Abdalla Hamid alipotembelea Tawi letu mwezi Juni 2025 na kufanya mkutano na wanachama wa Tawi la CCM China na kutoa darasa la itikadi na uongozi kwa wanachama waliohudhuria mkutano huo uliofanyika katika Mji wa Beijing.

**14. KUONGEZEKA KWA IDADI YA WANACHAMA**

Kupitia ushirikiano na viongozi wa mashina tumeendelea kuwatambua na kuwasajili wanachama na kuongeza idadi ya wanachama kwenye Tawi lake kutoka wanachama hai 200 Julai 2025 hadi wanachama 297 Disemba 2025.

**CHANGAMOTO**

Kama tunavyofahamu kwenye kila penye mafanikio hapakosi changamoto. Katika kipindi cha uongozi wetu tumekutana na baadhi ya changamoto kama ifuatavyo:

1. Ushiriki hafifu wa shughuli za Tawi na mashina kwa baadhi ya viongozi walipewa dhamana na wanachama kwenye mashina. Hii imesababishwa aidha na ubize wa shughuli binafasi za viongozi au wanachama na hivyo kutotoa kipaumbele kwa shughuli za kichama zinazohitaji kujitoa kwa muda ili kufanikiwa kwa shughuli hizo.

2. Kuwepo na mgongano wa kimaslahi kwa baadhi ya viongozi ngazi ya mashina na viongozi wa Tawi. Mgongano huu unatokea pale viongozi wanapofautiana kimtazamo wa namna bora ya kufanya juu ya jambo fulani kwa manufaa mapana ya chama.
3. Kusitishwa kwa muda kwa shughuli za kichama ndani ya tawi na mashina yake kutokana na sababu namba 2 hapo juu. Kusitishwa kwa shughuli hizi kulisababisha kuzorota kwa baadhi ya shughuli na kushusha morali kwa baadhi ya viongozi na wanachama.

**USHAURI KWA VIONGOZI WAJAO**

1. Kuendeleza umoja na mshikamano wa wanachama na viongozi kwani mgawanyiko hasa kipindi hiki ni mkubwa.
2. Kuendeleza na kubuni vyazo vya mapato ndani ya tawi na mashina yake ili kuweza kumudu gharama za uendeshaji wa shughuli za tawi na mashina yake.
3. Kuendelea kuboresha na kuweka kumbukumbu sahihi ya wanachama hai wa tawi kwa muda wote wa uongozi pamoja na kuendelea kusajili wanachama wapya.
4. Kuendelea kuisimamia katiba ya chama na miongozo mingine kwa kipindi chote cha uongozi ujao.
5. Kuweka wazi taarifa za mapato na matumizi ya Tawi na mashina yake
6. Kuongeza idadi ya mashina ikiwezekana popote palipo na mkusanyiko rasmi wa watanzania ndani ya mji husika kuwe na shina la Chama.
7. Kutatua migogoro inayoweza kuibuka ndani ya uongozi kwa kuwashirikisha watu watakaoweza kushauri pande zote mbili kwa manufaa mapana ya chama na wanachama wake bila kuegemea upande wowote.
8. Kuendelea kuihubiri amani, haki, upendo na mshimakamano wa watanzania na Tanzania kwani hatuna nchi nyingine ya kurudi tunayoweza kuiita 'NYUMBANI' tunapoamaliza masomo zaidi ya Tanzania.
9. Kuendelea kuwa wavumilivu kipindi cha changamoto na misukusuko, kufanya maamuzi kwa busara na kumtanguliza mungu mbele wakati wote.

**Taarifa hii imesomwa na Mwenyekiti wa Tawi kwenye mkutano Mkuu wa Tawi mbele ya wanachama wote leo tarehe 07.12.2025**

**Kidumu Chama Cha Mapinduzi.**






**Renatus Mahuyu**
**Katibu wa CCM Tawi la China**
**Tarehe: 06/12/2025**